Ujasiri Wakati Wa Huduma Ya Dhabihu

na

Ellis P. Forsman

Ujasiri Wakati Wa Huduma Ya Dhabihu

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 11, 2011

Ujasiri Wakati Wa Huduma Ya Dhabihu

2 Kor. 4:8-15

2 Kor. 4:8-15, "*Pande zote twadhikika bali hatusongwi twaona shaka bali hatukati tama; twaudhiwa bali hatuachwi, twatupwa chini bali hatuangamizwi; siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu. Kwa maana sisi tulio hai siku zote twatolewa tufe kwa ajili ya Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu ipatikanayo na mauti. Basi hapo mauti hufanya kazi ndani yetu, bali uzima ndani yenu. Lakini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani; kama ilivyoandikwa, Naliamini na kwa sababu hiyo nalinena; sisi nasi twaamini, na kwa sababu hiyo twanena; tukijua ya kwamba yeye aliyemfufua Bwana Yesu atatufufua sisi nasi pamoja na Yesu, na kutuhudhurisha pamoja nanyi. Kwa maana mambo yote ni kwa ajili yenu, ili neema hiyo ikiongezwa sana, kwa hao walio wengi shukurani izidishwe, na Mungu atukuzwe.*"

Paulo anaonyesha tabia tunayohitaji wakati tunapofanya kazi ya Bwana – hasa kazi ngumu. Tunaweza kujifunza kutokana na mfano wake.

Anazungumzia mchezo wa riadha kuonyesha hatua jinsi alivyo jaribu. Hebu na tuangalie ujasiri wake, ni ujasiri upi unaweza kuwa wetu.

Ujasiri wa Paulo unaonekana katika ulinganifu wake

Twadhikika pande zote, bali hatusongwi.

2 Kor. 4:8, "Pande zote twadhikika bali hatusongwi; twaona shaka bali hatukati tamaa;"

Tunasumbuliwa (kandamizwa) – (Kiyunani kukusanya; au kama kukamua karatasi.

Mahubiri ya Paulo yalikuwa kama mkusanyiko mkubwa wa watu wakimwendea. Lakini mkusanyiko ambao Paulo anaongelea hapa ulikusudia kumdhuru.

Hatukati tama (hatusongwi) – wakati mwingine katika mkusanyiko kama huo ni vigumu hata kupumua.

Paulo alikumbana na hili kwa nyakati. Ndivyo itakavyokuwa kwetu kwa nyakati tofauti. Huduma mara nyingi sio rahisi.

Mungu alimsaidia Paulo kutoka katika hali ngumu kama hizo.

Tunaujasiri kwamba Mungu atatuondoa tutoke katika kundi la watu.

Kuteswa – hatuna njia nyingine, katika kupoteza fahamu.

Paulo alikuwa katika hali tofauti wakati ambapo angeweza kupoteza fahamu. Kwa nyakati hii itatutokea.

Sio katika mateso – Paulo alikuwa na ujasiri kwamba Mungu atamshindania hali yo yte ngumu. Hii inapaswa kuwa ujasiri wetu katika huduma ya Mungu.

Mungu yu pamoja nasi.

Twaudhiwa, bali hatuachwi.

2 Kor. 4:9, "*Twaudhiwa, bali hatuachwi twatupwa chini, bali hatuangamizwi.*"

Twaudhiwa – Sawa kuwinda na kufukuza mnyama wa porini.

Mateso ya Paulo hayakukoma. Mdo. 23:12, "*Kulipopambazuka, Wayahudi wakafanya mapatano, wakajifunga kwa kiapo kwamba hawatakula wala hawatakunywa mpaka wamwue Paulo.*"

Nasi tunaweza kuhisi hivyo katika kazi yetu ya huduma.

Hatuachwi – Kusahau au kutoka.

Paulo hakujisikia kama ameachwa. Ebr. 13:5, "Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mlivyo navyo kwa kuwa yeye mwenyewe amesema sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa."

Lazima tumwamini Mungu katika ahadi hii. Tutafanya mambo makuu kama tukikumbuka hili.

Twatupwa chini, bali hatuangamizwi.

2 Kor. 4:9, "*Twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini bali hatuangamizwi;*"

Twatupwa chini (Kandamizwa chini) – Kutupwa chini, au kugongwa.

Paulo alikumbana na mambo mengi yaliyomtupa chini mara nyingi. Mambo kama hayo yatakuwa yetu kwa nyakati tofauti.

Hatuangamizwi – Kuteketezwa; kuangamizwa.

Paulo alitupwa chini, bali sio nje. Mdo14:19, "*Lakini Wayahudi wakafika toka Antiokia na Ikonio, wakawashawishi makutano hata*

wakampiga kwa mawe Paulo, wakamburuta nje ya mji wakidhani ya kuwa amekwisha kufa."

Tutakuwa na mwangaza wetu, lakini Mungu ataturudisha tena.

Ujasiri katika nafasi ya kutumika

2 Kor. 4:10, "*Siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu.*"

Ilikuwa ni nafasi ya Paulo kauteseka kama alivyofanya Bwana wake Yesu; kila mara akibeba katika mwili wake kifo cha Bwana Yesu. Aliteseka kwa kubeba huduma kama Bwana wake alivyofanya.

- 1 Kor. 15:31, "*Naam, ndugu kwa huku kujisifu kwangu niliko nako juu yenu katika Kristo Yesu Bwana wetu, ninakufa kila siku.*"
- Rum. 8:36, "*Kama ilivyoandikwa ya kwamba, kwa ajili yako tunauawa mchana kutwa, tumehesabiwa kuwa kama kondoo wa kuchinjwa.*"

Ili kwamba maisha ya Yesu yaweze kuonekana katika miili yetu. 2 Kor. 4:11, "*Kwa maana sisi tulio hai, sikuzote twatolewa tufe kwa ajili ya Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu ipatikananyo na mauti.*"

Ilikuwa ni nafasi kwa ajili ya Paulo kuzalisha katika maisha yake maisha ya Bwana wake.

Sasa kifo kinatenda kazi ndani yetu, bali uzima ndani yenu. 2 Kor. 4:12, "*Basi hapo mauti hufanya kazi ndani yetu, bali uzima ndani yenu.*"

Paulo alikuwa na furaha kwamba kifo chake cha kila siku ilizaa uzima wa Kristo katika maisha yaw engine).

Ujasiri upo katika imani

2 Kor. 4:13, "*Lakini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani; kama ilivyoandikwa, naliamini, na kwa sababu hiyo nalinena; sisi nasi twaamini; na kwa sababu hiyo twanena;*"

Paulo anatoa nukuu katika Zaburi 116:10, "*Naliamini, kwa maana nitasema, Mimi naliteswa sana.*"

Anasema kwamba anatumaini ile ile kama ya Daudi. Imani ya Daudi ilikuwa na nguvu kwamba angeweza kuitangaza bila kujali kile ambacho maadui zake wangefanya. Paulo aliamini na hivyo akasema.

Yer. 20:9, "*Nami nikisema sitamtaja wala sitasema tena kwa jina lake; basi ndipo moyoni mwangu kumekuwamo kama moto uwakao,*

uliofungwa ndani ya mifupa yangu, nami nimehoka kwa kustahimili, wala siwezi kujizuia."

Mafanikio yetu yatajuwa sambamba na imani yetu. 1 Yoh. 5:4, "*Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu.*"

Ujasiri katika tumaini ya ufufuo

2 Kor. 4:14, "*Tukijua ya kwamba yeye aliyemfufua Bwana Yesu, atatufufua sisi nasi pamoja na Yesu, na kutuhudhurisha pamoja nanyi.*"

Paulo aliamini katika ufufuo wa Kristo. Akaamini kwamba watenda kazi wanaojitoa dhabihu pia watafufuliwa. Hata kama Paulo alikufa, anaamini kwamba Mungu atamfufua kwenda mbinguni. Hiyo ilimpa ujasiri.

Paulo alikuwa na furaha kwamba Wakorintho wangekuwa pamoja naye katika ufufuo. Hiyo inaweza kutufanya nasi tuwe na furaha.

Ujasiri katika ufufuo unatufanya tupitie wakati mgumu.

Ujasiri upo katika kutazama mafanikio ya kazi ya dhabihu

2 Kor. 4:15, "*Kwa maana mambo yote ni kwa ajili yenu, ili neema hiyo ikiongezwa sana, kwa hao walio wengi shukrani izidishwe na Mungu atukuzwe.*"

Hataivyo Paulo aliteswa kwa sababu ya kuhubiri, alikuwa anapata mafanikio. Aliwahubiria Wakorintho, na wakaamini. Neema ya Mungu ilikuwa ikitangazwa katika dhabihu yake ya kuhubiri. Paulo alikuwa na furaha kujitoa dhabihu kuwaleta wengi kwa Bwana wake Yesu. Shukrani zilizotolewa zilitoka katika mioyo ya wengi kwa sababu ya hili.

Ndivyo itakavyokuwa hata leo tunapotangaza injili.

Hitimisho

Huduma ya Bwana inaweza kuwa ngumu. Tunapaswa kuihesabu kwamba ni nafasi ya kumtumikia Bwana bila kujali kuwa ina ugumu kiasi gani. Tuna ujasiri kwamba Mungu atakuwa pamoja nasi muda wote. Tunafuraha tunapoona wengine wakiokolewa, tukiwa na matumaini ya ufufuo.